

Amri za Kanisa: Mambo ya Muhimu kujua na Kuzingatia

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 19, 2016

Mafundisho ya Katekismus · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Amri za Kanisa

Amri za Kanisa ni zipi?

Amri za kanisa ni; 1. Hudhuria Misa Takatifu Dominika na sikukuu zilizoamriwa. 2. Funga siku ya Jumatano ya Majivu; usile nyama siku ya Ijumaa Kuu 3. Ungama dhambi zako walau mara moja kila mwaka. 4. Pokea Ekaristi Takatifu hasa wakati wa Pasaka 5. Saidia Kanisa Katoliki kwa zaka 6. Shika sheria Katoliki za ndoa.

Katika Amri ya kwanza ya Kanisa tumeamriwa nini?

Tumeamriwa tusikilize Misa kila siku ya Mungu na Sikukuu zilizoamriwa.

Sikukuu zilizoamriwa ni zipi?

Ndizo:

Katika Amri ya Kwanza ya kanisa tumekatazwa nini?

Tumekatazwa; 1. Kukosa Misa 2. Kufanya kazi nzito siku hizo

Kujinyima ni nini?

Kujinyima ni kujikatalia kitu ukipendacho mfano nyama, pombe, sigara, muziki, safari, maongezi n.k.

Nani ana lazima ya kufunga?

Kila Mkristo aliyetimiza miaka 14 na zaidi anapaswa kufunga kula nyama (Ijumaa kuu) na mwenye miaka zaidi ya 21 kufunga chakula. (Jumatano ya Majivu)

Siku za kufunga ni zipi? Na siku gani tumekatazwa kula nyama?

Siku za kufunga ni Jumatano ya majivu, siku za Kwaresima isipokuwa Dominika zake, na siku iliyokatazwa kula nyama ni siku ya Ijumaa kuu.

Katika Amri ya Tatu ya Kanisa tumeamriwa nini?

Katika Amri ya Tatu ya Kanisa tumeamriwa kuungama mara kwa mara walau mara moja kila mwaka

Katika Amri ya Nne ya Kanisa tumeamriwa nini?

Katika Amri ya Nne ya Kanisa tumeamriwa tupokee Ekaristi Takatifu walau mara moja kwa mwaka wakati wa pasaka.

Katika Amri ya Tano ya Kanisa tumeamriwa nini?

Katika Amri ya Tano ya Kanisa tumeamriwa kufahamu kuwa gharama za dini na za mapadre zatupasa. Yaanai wakristo walitegemeze Kanisa na wahudumu wake na hasa katika kazi ya kueneza injili.

Zaka ni nini?

Zaka ni asilimia kumi (10%) ya pato la mtu kwa mwaka ambalo anapaswa kulitoa kwa Kanisa.

Asiyelipa Zaka na michango mingine ya Kanisa ya lazima atenda dhambi gani?

Atenda dhambi kubwa: Yampasa kulipa na kuungama.

Amri ya Sita ya Kanisa Inadai nini?

Inadai kushika Sheria Takatifu Za ndoa

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=498>